

MKATABA WA UPANGAJI (LEASE AGREEMENT)

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 30/1/2026 INVOICE: S03/0326

KATI YA

Rose S. Mihayo wa S.L.P 914, Dar es Salaam, ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGISHAJI", kwa upande mmoja;

NA

SUNCOM OIL LIMITED wa S.L.P 6380, Dar es Salaam, ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGAJI", kwa upande mwingine.

UTANGULIZI (RECITALS)

KWA KUWA Mpangishaji ni mmiliki halali wa eneo la biashara lililopo Goba - Dar es Salaam;

NA KWA KUWA Mpangaji ameomba kupangisha eneo hilo kwa madhumuni ya biashara;

NA KWA KUWA pande zote zimekubaliana kwa hiari yao bila shuruti yoyote kuingia makubaliano haya;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia masharti na makubaliano yafuatayo, pande zote zinakubaliana kama ifuatavyo:-

1. MUDA WA UPANGAJI

1.1 Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia tarehe 01/03/2026 hadi tarehe 28/02/2031.

2. KODI YA PANGO NA NAMNA YA MALIPO

2.1 Kodi ya pango itakuwa Shilingi Milioni Tano na Laki Nne tu (TZS 5,400,000/-) kwa mwaka.

2.2 Mpangaji atalipa kodi hiyo mwaka mmoja mmoja mapema kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa upangaji.

2.3 Malipo ya kila mwaka yatathibitishwa kwa stakabadhi au uthibitisho wa maandishi utakaosainiwa na pande zote.

3. WAJIBU WA MPANGAJI

Mpangaji atawajibika:-

4. WAJIBU WA MPANGISHAJI

Mpangishaji atawajibika: -

- a) Kukabidhi eneo katika hali nzuri kabla ya kuanza kwa upangaji.
- b) Kutomwingilia Mpangaji endapo ametimiza masharti yote ya mkataba huu.

5. KUSITISHA MKATABA

5.1 Endapo Mpangaji atasitisha mkataba huu kabla ya muda wake kuisha kwa sababu zake binafsi, hatakuwa na haki ya kurejeshewa kodi aliyolipa.

5.2 Endapo Mpangaji atashindwa kulipa kodi kwa wakati, Mpangishaji atatoa notisi ya siku thelathini (30), na kushindwa kulipa ndani ya muda huo kutampa Mpangishaji haki ya kusitisha mkataba huu.

6. KUONGEZA MUDA WA MKATABA

6.1 Mpangaji atakayehitaji kuongeza muda wa upangaji atatoa notisi ya maandishi siku thelathini (30) kabla ya kumalizika kwa mkataba huu.

6.2 Masharti mapya ya upangaji yatajadiliwa na kukubaliwa kwa maandishi na pande zote.

SAHIHI ZA WAHUSIKA

IMESAINIWA NA:

Rose S. Mihayo

Rose S. Mihayo

(MPANGISHAJI)

Tarehe: 25/01/2026

[Signature]

Kwa niaba ya SUNCOM OIL LIMITED

(MPANGAJI)

Tarehe: 25/01/2026

MBELE YA SHAHIDI:

Jina: NEEMA VEDASTUS

Anuani: SILP 2005

Sahihi: Ngagangh

Cheo: WAKILI

Tarehe: 25/01/2026

